

### KILA MTENDA FADHILA

- |   |  |
|---|--|
| <p>1. Wa Bara na wa Mwambao, na wote mlio mbali.<br/>Nawaiteni kikao, tuongee Kiswahili.<br/>Kwa kila siku uchao, huzaa lile na hili.<br/>Kila mtenda fadhila, malipo yake kilio.</p> <p>2. Malipo yake kilio, kilamtenda fadhila.<br/>Kuna mengi matukio, yavurugayo akili.<br/>Tegesha sana sikio, ishike sana vikali.<br/>Kila mtenda fadhila, malipo yake kilio.</p> <p>3. Mwendo huu wa kileo, yafaa kutafakari.<br/>Una mengi matokeo, hasa yaliyo dhalili.<br/>Nia na mategemeo, sikilizeni kauli.<br/>Kila mtenda fadhila, malipo yake kilio.</p> <p>4. Enyi wema mfanyao, kuacha msikubali.<br/>Una hiba na mafao, na faraja mbalimbali.<br/>Wema hauna makwao, wema kinga ya mwili.<br/>Kila mtenda fadhila, malipo yake kilio.</p> | <p>5. Japo nakubali ndio, wema kufanya halali.<br/>Walakini basi sio kupitiliza mbali.<br/>Wema una matukio, ndio chanzo cha muhali.<br/>Kila mtenda fadhila, malipo yake kilio.</p> <p>6. Nduguzo wape makao, wafae kwelikweli.<br/>Wapende watoto wao, itakupata dhohali.<br/>Hii ni asili yao, haramu kwao halali.<br/>Kila mtenda fadhila, malipo yake kilio.</p> <p>7. Wema una maumbo, kwa majibu na maswali.<br/>Na kuchaniana nguo, kuraruana miili.<br/>Sipendi mwenendo huo, ni mwenendo wa mshazali.<br/>Kila mtenda fadhila, malipo yake kilio.</p> <p>8. Hapo naweka kituo, mungule siendi mbali.<br/>Kiumbe hilo chaguo, lenye mwanga wa kadili.<br/>Nimefikia upeo, kuwapeni taamuli.<br/>Kila mtenda fadhila, malipo yake kilio.</p> |
|---|--|

*Jumanne Mungule,  
S.L.P. 63281  
Pugu - Kisumu.  
(Limetoka kwenye Mwananchi, Jumanne Julai 23,  
2002, uku.20)*